MAKALA NO.

03

سلسلة في أحكام الصيام

MFULULIZO WA HUKMU ZA SWAUMU

1. SHARTI ZA KUKALIFISHWA FUNGA

2. MAMBO YA WAJIBU KATIKA FUNGA YA MWEZI WA RAMADHANI

MWANDISHI:

ABUU ZAKARIYYAA YAHYA IBN HASSAN AL-HAMBALIY

UNGUJA - TANZANIA

UTANGULIZI

Kila sifa njema anastahiki Allah mola mlezi wa viumbe vyote na sala na salamu zimfikie Mtume wetu Muhammad, ahli zake, maswahba zake na wale wote waliowafuata kwa wema.

Ama baada ya utangulizi, katika Makala hii, tutaangalia katika kigawanyo cha pili cha sharti za swaum, ambacho ni sharti za kukalifishwa mtu kufunga swaum na pia tutaangalia mambo ya wajibu katika swaum

2) SHARTI ZA KUKALIFISHWA (KULAZIMISHWA) MTU KUFUNGA RAMADHANI

Ama sharti za kukalifishwa mtu kufuga ni tatu (3): -

(a) Uwezo wa kufunga
(b) Kuwa mkaazi
(c) Kufika umri wa kubalehe au kuvunja ungo

MAELEZO YA SHARTI ZA KUKALIFISHWA KUFUNGA

(a) Uwezo wa kufunga

Allah mtukufu ameifanya sheria yake kuwa ni nyepesi kufanyika kwa mwaanadam, sababu ni sharia ambayo inaendana na maumbile ya mwanaadam

Allah mtukufu anasema

لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفۡسًا إِلَّا وُسۡعَهَا ﴿٢٨٦﴾ البقرة [286]

Allah haikalifishi nafsi isipokuwa kwa kadri iwezavyo

Amesema Imam Al-Qurtuby katika kuifasiri aya hii

نَصَّ اللَّهُ تَعَالَى عَلَى أَنَّهُ لَا يُكَلِّفُ الْعِبَادَ مِنْ وَقْتِ نُزُولِ الْآيَةِ عِبَادَةً مِنْ أَعْمَالِ الْقَلْبِ أَوِ الْجَوَارِحِ إِلَّا وَهِيَ فِي وُسْعِ الْمُكَلَّفِ وَفِي مُقْتَضَى إِدْرَاكِهِ وَبِنْيَتِهِ

Ameainisha Allah mtukufu juu ya kwamba, hawakalifishi waja ibada wakati wa kushuka aya, katika matendo ya moyo au viwiliwili isipokuwa katika uwezo wa aliyekalifishwa, na katika muktadha wa kudiriki kwake na kuanzisha (haya matendo)[1]

Hivyo basi, kwa mtu asiyeweza kufunga kama vile mgonjwa, mzee sana n.k hawa hawajalazimishwa na sheria kufunga

(b) Kuwa mkaazi

Msafiri ambaye ni kinyume cha mkaazi, huyu sheria haijamlazimisha kufunga, kama alivyosema Allah mtukufu

[1] Al-jaamiu liahkaamil Qur-an 3/429 (shaamila)

﴿ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ﴾ البقرة [184]

Basi na yeyote atakaye kuwa miongoni mwenu ni mgonjwa au yupo safarini, basi atimize hesabu katika masiku mengineyo

Basi ikafahamika kwa aya hii kuwa aliyesafirini hajalazimishwa kufunga, kwa maana ambaye ni mkaazi basi analazimishwa na sheria kufunga

(c) Kufika umri wa kubalehe au kuvunja ungo

وعن علي رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم ((رُفِعَ القلم عن ثلاثةٍ: عن النَّائم حتى يستيقظَ، وعن الصَّبيِّ حتى يَحتَلِمَ، وعن المجنونِ حتى يَعقِلَ))

Kutoka kwa Aliy Allah amridhie amesema: amesema mjumbe wa Allah juu yake sala na salamu: Kalamu imenyanyuliwa kwa watu wa sampuli tatu; aliyelalala mpaka atakapoamka, na mtoto mpaka atakapo balehe, na mwendawazimu mpaka atakapo kuwa na akili[2]

Mtume juu yake sala na salamu ametaja moja katika watu ambao hawaandikiwi amali zao ni mtoto mpaka atakapo balehe, kutoandikiwa matendo yake ni dalili ya kuwa sheria haijamlazimu kutenda ibada.

MAMBO YA WAJIBU KATIKA SWAUM YA RAMADHANI

Maana ya wajibu kisheria: Ni jambo ambalo sheria imeliamrisha katika namna ya kulilazimisha kufanywa

Mambo ya wajibu katika swaum ni manane (8): -

(i) Uwajibu wa kuutafuta mwezi mwandamo, uwajibu wa kutoshelezana

Swaum ya Ramadhani imefungamanishwa katika kuanza kufunga kwake na kumaliza kwa kuonekana mwezi au kukamilisha siku thalathini za mwezi baada ya mwezi kutokuonekana baada ya siku ishirini na tisa, kama ilivyokuja katika hadithi

وعن ابْنَ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: «إِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَصُومُوا، وَإِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَأَفْطِرُوا، فَإِنْ غُمَّ عَلَيْكُمْ فَاقْدُرُوا لَهُ»

“Na kutoka kwa Ibn Umara (Allah amridhie na baba yake), amesema: Nilimsikia mjumbe wa Allah juu yake sala na salam amesema: ((Pindi mtakapouona [mwezi mwandamo wa ramadhani] fungeni, na pindi mtakapouona [mwezi mwandamo wa shawwaal] basi fungueni, na ikiwa kuna mawingu ukadirieni [kwa siku thalathini za shaaban au thalathini za shawwaal]))”[3]

[2]Sunan Abii Daud hadith no.4403
[3] Sahihu Al-bukhary 1900 na Sahihu Al-muslim 1080

Na uwajibu huu wa kuutafuta mwezi ni wa kutoshelezana, kwa maana wakiuona watu wachache waaminifu basi inatosha kwa wengine kufunga na si kila mtu lazima auone

KATIKA KIPENGELE HIKI, TUTAYATIZAMA MAMBO YAFUATAYO: -

(A) WATU WANGAPI INAFAA KUWA MASHAHIDI KATIKA KUONA MWEZI MWADAMO WA RAMADHANI AU SHAWWAAL

Ama kauli yenye nguvu na Allah ni mjuzi zaidi, ni kwamba inatosha shahidi mmoja wakati wa kuingia mwezi wa Ramadhani, na mashahidi wawili wakati wa kuingia miezi mingine

Ama dalili ya kuonesha kuwa wakati wa kuingia Ramadhani inatosha shahada ya mtu mmoja

عن ابنِ عمر، قال: تراءى الناسُ الهِلالَ، فأخبرتُ رسولَ الله –صلَّى الله عليه وسلم– أني رأيتُه فَصَامَ وأمَرَ النَّاسَ بِصِيَامِهِ

Kutoka kwa ibnu Umara (Allah amridhie), amesema; watu walioneshana mwezi mwandamo, nikampa habari Mtume (Sala na salamu zimfikie) ya kwamba mimi nimeuona, (Mtume) akafunga na akaamrisha watu wafunge[4]

Ama dalili ya shahada ya watu wawili ikiingia miezi mingineyo

قال حُسَيْنُ بْنُ الْحَارِثِ الْجَدَلِيُّ، مِنْ جَدِيلَةَ قَيْسٍ، أَنَّ أَمِيرَ مَكَّةَ خَطَبَ، ثُمَّ قَالَ: «عَهِدَ إِلَيْنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ نَنْسُكَ لِلرُّؤْيَةِ، فَإِنْ لَمْ نَرَهُ، وَشَهِدَ شَاهِدَا عَدْلٍ نَسَكْنَا بِشَهَادَتِهِمَا»

Amesema Husayn Ibn Al- haarith Al-jadaly, kutoka katika kabila la Qays, ya kwamba Amiri wa Makka alihutubia kisha akasema: (Alituusia sisi mjumbe wa Allah juu yake sala na salamu, tufanye ibada kwa kuona mwezi, na endapo tusipouona, na wakatoa ushuhuda mashahidi wawili waadilifu, tutafanya ibada kwa ushahidi wao)[5]

Hadithi ya mwanzo ya Ibn Umara ni maalumu kwa kuingia mwezi wa Ramadhani, na ya Amir wa Makka inaenea kwa miezi yote, Hivyo haitokubalika kauli ya mtu mmoja kwa mwezi mwandamo wa shawwaal.

(B) SHAHADA YA MWANAMKE KATIKA KUONA MWEZI

Shahada ya mwanamke katika kuona mwezi haikubaliki. Amesema Imam An-nawawiy

وَاتَّفَقُوا عَلَى أَنَّ (أَصَحَّهُمَا) أَنَّهُ شَهَادَةٌ فَعَلَى هَذَا لَا يُقْبَلُ فِيهِ الْعَبْدُ وَالْمَرْأَةُ وَنَصَّ عَلَيْهِ فِي الْأُمِّ

Na wamekubaliana (wanachuoni) juu ya kwamba lililo sahihi mno katika kauli mbili ni kwamba habari ya kuona mwezi ni shahada, na juu ya hili, haikubaliki kauli ya mtumwa na **mwanamke**, na ameitaja (kauli hii, Imam Shaafiy) katika Al-ummu[6]

[4] Sunan Abii Daud, Hadithi no.2342
[5] Sunan Abii Daud, Hadith no.2338
[6] Al-majmuu 6/277 (Shaamila)

(C) SHAHADA YA MTOTO MWENYE UWEZO WA KUPAMBANUA MAMBO, KATIKA KUONA MWEZI

(وَأَمَّا) الصَّبِيُّ الْمُمَيِّزُ الْمَوْثُوقُ بِهِ فَلَا يُقْبَلُ قَوْلُهُ إنْ شَرَطْنَا اثْنَيْنِ أَوْ قُلْنَا شَهَادَةٌ وَهَذَا لَا خِلَافَ فِيهِ (وَإِنْ قُلْنَا) رِوَايَةٌ فَطَرِيقَانِ (الْمَذْهَبُ) وَبِهِ قَطَعَ الْجُمْهُورُ لَا يُقْبَلُ قَطْعًا

Na ama mtoto mwenye uwezo wa kupambanua mambo, mwenye kuaminika, basi kauli yake haikubaliki endapo tukiweka sharti la pili au tukisema (kauli yake ni) shahada, na hili halina khilafu (tofauti ya wanachuoni), na endapo tukisema (habari yake) ni riwaya, basi (hukmu) yake ina njia mbili katika madhehebu (ya imam shaafiy') na kwa kauli ambayo wamekata jumhuri (wengi katika wanachuoni) ni kwamba haikubaliki kauli yake[7]

(D) SHAHADA YA KAFIRI KATIKA KUONA MWEZI

Kafiri kauli yake haikubaliki katika kutoa ushahidi wa mwezi mwandamo, kama alivyo sema Imam An-nawawiy

وَأَمَّا) الْكَافِرُ وَالْفَاسِقُ وَالْمُغَفَّلُ فَلَا يُقْبَلُ قَوْلُهُمْ فِيهِ بِلَا خِلَافٍ

Na ama kafiri, au fasiq (mtu muovu) na mwenye kughafilika kauli zao hazikubaliki bila tofauti ya (wanachuoni)[8]

(E) KUFAHAMU KUINGIA KWA MWEZI KWA NJIA YA KALENDA

Ama kutumia kalenda katika kujua kuingia mwezi pasi na kuzingatia mwandamo wa mwezi au kukamilisha siku thalathini ya mwezi ni jambo ambalo halifai. Amesema Ibnu Daqiiq Al-I'id (Allah amrehem)

والذي أقول به أن الحساب لا يجوز أن يعتمد عليه في الصوم لمفارقة القمر للشمس على ما يراه المنجمون من تقدم الشهر بالحساب على الشهر بالرؤية بيوم أو يومين فإن ذلك إحداث لسبب لم يشرعه الله تعالى

Na lile ambalo nasema kwalo ni kwamba, Kalenda haijuzu kuizingatia katika swaum, kwa kulinganisha mwezi na jua kwa kile ambacho wanakiona wanajimu, kutokana na kutangulia mwezi kwa kuhesabu mwezi kwa njia ya mwandamo kwa siku moja au mbili, hakika hilo ni kuzusha sababu Allah hakuiweka katika sheria[9]

[7] Al-majmuu 6/277 (Shaamila)
[8] Al-majmuu 6/277 (Shaamila)
[9] Ihkaamul ahkaam, sharhu umdatul ahkaam, uk. 268 Chapa ya mwaka 2005M, Muassasatur risaalat

(F) KUTUMIA DARUBINI KUANGALIA MWEZI MWANDAMO

Amesema Sheikh Ibnu Uthaymiin Allah amrehemu

وأما استعمال ما يسمى «بالدربيل» وهو المنظار المقرب في رؤية الهلال فلا بأس به، ولكن ليس بواجب، لأن الظاهر من السنة أن الاعتماد على الرؤية المعتادة لا على غيرها. ولكن لو استعمل فرآه من يوثق به فإنه يعمل بهذه الرؤية، وقد كان الناس قديماً يستعملون ذلك لما كانوا يصعدون المنائر في ليلة الثلاثين من شعبان، أو ليلة الثلاثين من رمضان فيتراءونه بواسطة هذا المنظار، وعلى كل حال متى ثبتت رؤيته بأي وسيلة فإنه يجب العمل بمقتضى هذه الرؤية، لعموم قوله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «إذا رأيتموه فصوموا، وإذا رأيتموه فأفطروا»

Ama kutumia Darubini ambayo ni kioo cha kukaribisha (vitu vilivyo mbali) katika kuangalia mwezi mwandamo, (jambo hili) halina ubaya, lakini sio wajibu, kwa sababu lililo la dhahiri katika sunna ni kwamba mazingatio ni katika mwezi uliozoeleka na si mwingineo, lakini lau akiitumia (mtu darubini) akauona (mwezi mwandamo) yule mwenye kuaminika, basi utafanyiwa kazi uonaji huu. Na walikuwa watu zamani wanatumia hilo pale walipokuwa wakipanda minara katika usiku wa thalathini shaaban, au usiku wa thalathini Ramadhani na wanaoneshana mwezi kwa njia ya hiki kioo (Darubini). Na juu ya kila hali, pindi utakapo onekana (mwezi) kwa njia yoyote, basi inawajibu kufanyia kazi kwa muktadha wa uonaji huo, kwa kuenea kauli ya Mtume juu yake sala na salamu (Pindi mtakapo uona fungeni na mtakapo uona fungueni)[10]

(G) WAKIONA MWEZI WATU WA MJI FULANI, JE! INALAZIMU WATU WA MIJI MINGINE KUFUNGA AU KUFUNGUA?

Katika jambo hili wanachuoni wametofautiana katka kauli nane (8) kama alivyotaja Swiddiq Ibn Hassan Khan katika (Ar rawdhatu An-nadiyyah, uk. 225 Juzuu 1 Chapa Daarul maa'rifa). Lakini kauli ambazo zimeenea au zimekuwa mashuhuri ni tatu (3) ambazo ni: -

KAULI YA KWANZA: Ukionekana mwezi sehemu yeyote basi ina wajibu watu wote kufunga. Na hii ni Kauli ya Imaam Maalik, Shaafiy, Ahmad, Allayth, Ibn Taymiyyah, Shawkaaniy, Swiddiiq ibn Hassan Khaan, Albaaniy na wengineo.

KAULI YA PILI: Ukionekana mwezi na watu wa mji fulani basi ni lazima kufunga watu wanao endana katika machomozo ya mwezi. Na hii kauli katika Madhehebu ya Imaam Shaafiy, Sheikh Muqbil na Ibn Uthaymiin

KAULI YA TATU: Watu watafunga endapo mwandamo wa watu wengine utakubalika mbele ya kiongozi mkuu.

[10] Majmuul fataawa wa Rasailul Al-uthaymiin

Katika kauli zote hizi tatu, dalili ambazo wanazotumia ni zile zile isipokuwa namna ya kuzitumia dalili hizo, Ama dalili hizo ni kama ifuatavyo;

DALILI YA KWANZA: Ni kauli ya Allah mtukufu

﴿ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُ ﴾ البقرة [185]

Na yeyote atakaye shuhudia miongoni mwenu mwezi (wa Ramadhani) basi na afunge

DALILI YA PILI: ni kauli ya Mtume Juu yake sala na salamu

«صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ، فَإِنْ غُمِّيَ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا الْعَدَدَ»

Fungeni kwa kuonekana mwezi (mwandamo) na fungueni kwa kuonekana kwake, na endapo mawingu yakitanda, basi kamilisheni idadi[11]

DALILI YA TATU: Ni Hadithi ya Kurayb

عَنْ كُرَيْبٍ، أَنَّ أُمَّ الْفَضْلِ بِنْتَ الْحَارِثِ، بَعَثَتْهُ إِلَى مُعَاوِيَةَ بِالشَّامِ، قَالَ: فَقَدِمْتُ الشَّامَ، فَقَضَيْتُ حَاجَتَهَا، وَاسْتُهِلَّ عَلَيَّ رَمَضَانُ وَأَنَا بِالشَّامِ، فَرَأَيْتُ الْهِلَالَ لَيْلَةَ الْجُمُعَةِ، ثُمَّ قَدِمْتُ الْمَدِينَةَ فِي آخِرِ الشَّهْرِ، فَسَأَلَنِي عَبْدُ اللهِ بْنُ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا، ثُمَّ ذَكَرَ الْهِلَالَ فَقَالَ: مَتَى رَأَيْتُمُ الْهِلَالَ؟ فَقُلْتُ: رَأَيْنَاهُ لَيْلَةَ الْجُمُعَةِ، فَقَالَ: أَنْتَ رَأَيْتَهُ؟ فَقُلْتُ: نَعَمْ، وَرَآهُ النَّاسُ، وَصَامُوا وَصَامَ مُعَاوِيَةُ، فَقَالَ: " لَكِنَّا رَأَيْنَاهُ لَيْلَةَ السَّبْتِ، فَلَا نَزَالُ نَصُومُ حَتَّى نُكْمِلَ ثَلَاثِينَ، أَوْ نَرَاهُ، فَقُلْتُ: أَوَ لَا تَكْتَفِي بِرُؤْيَةِ مُعَاوِيَةَ وَصِيَامِهِ؟ فَقَالَ: لَا، هَكَذَا أَمَرَنَا رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

Kutoka kwa Kurayb, kwamba, Ummul Fadhli bint Al-haarith, alimtuma (Kurayb) kwenda kwa Mua'wiya Shamu. Akasema (Kurayb): Nilifika Shamu, nikakidhi haja yake, na ukaandama mwezi wa Ramadhani na mimi nipo Shamu, basi nikauona mwezi usiku wa Ijumaa, kisha nikaingia Madina mwishoni mwa mwezi, akaniuliza mimi Abdullah ibn Abbaas (Allah amridhie yeye na baba yake), kisha akataja mwezi kisha akasema: Ni wakati gani mumeuona mwezi mwandamo? Nikasema: Tumeuona usiku wa ijumaa. Kisha akasema: wewe umeuona? Nikasema: ndio, na wakauona watu, na wakafunga na akafunga Mua'wiya. Akasema (Ibn Abbaas): lakini sisi tumeuona usiku wa jumaamosi, tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe siku thalathini au tuuone. Nikasema: Hivi hutosheki na uonaji wa Mua'wiya na funga yake? Akasema: Hapana, bali hivi ndivyo alivyo tuamrisha Mjumbe wa Allah juu yake sala na salamu[12]

[11] Sahihu Muslim, hadithi no. 1081
[12] Sahihu Muslim, hadithi no. 1087

HOJA YA KAULI YA KWANZA

- Kwa kutumia dalili ya kwanza na ya pili, ni kwamba; Maamrisho ya kufunga kwa kuonekana kwa mwezi na kufunga pindi watakapo shuhudia mwezi ni kauli yenye kuenea kwa watu wote bila ya kujali watu wa mji fulani pasi na mji mwingine

HOJA YA KAULI YA PILI

- Kwa kutumia dalili ya kwanza; ni kwamba wale wasiowafikiana katika machomozo ya mwezi basi wanakuwa hawaja shuhudia mwezi sio ki hakika wala ki hukumu, na Allah amewajibisha swaumu kwa aliyeshuhudia mwezi
- Kwa kutumia dalili ya pili; ni kwamba Allah amefungamanisha swaumu kwa kuona mwezi, na wale wenye kwenda tofauti katika machomozo wanakuwa hawajauona mwezi si ki hakika wala ki hukumu
- Ama kwa kutumia dalili ya tatu; na hii ndio dalili kubwa sana kwa watu wa kauli hii. Kwamba maneno ya Ibn Abbaas yanaonesha kuwa endapo kuna tofauti katika machomozo ya mwezi basi kila watu wafunge na wenye kuendana katika machomozo ya mwezi

HOJA ZA WATU WA KAULI YA KWANZA KWA WATU WA KAULI YA PILI

- Jambo la utofauti wa machomozo katika mwezi ni jambo lisilodhibitiwa na mipaka maalum, basi ni ipi mipaka maalum ya kujua tofauti ya machomozo ya mwezi?
- Makusudio ya aya na hadithi ambazo wametolea hoja watu wa kauli ya pili ni elimu juu ya kuingia mwezi wa Ramadhani, na limepatikana hilo kwa uonaji wa watu wa mji maalum, na kama vile ambavyo inalizimu kufunga watu wa mji fulani kwa uonaji wa baadhi ya watu katika mji huo, vilevile inapasa watu wa miji mingine kufunga kwa uonaji wa watu wa mji huo
- Ama majibu yao katika hadithi ya Kurayb
  - Ibn Abbaas hakuweka wazi kuwa Mtume (juu yake sala na salamu) amewaamrisha wasifanyie kazi uonaji mwezi mwandamo wa wengine, bali alikusudia Ibn Abbaas kuwa Mtume (juu yake sala na salamu) aliwaamrisha watimize siku thalathini au wauone mwezi kama ilivyokuja katika hadithi nyinginezo
  - Hadithi hii imekuja katika mlango wa yule ambaye amefunga kwa mwandamo wa mwezi wake kisha ikamjia yeye habari katikati ya Ramadhani kuwa mji mwingine wameuona mwezi kabla yao. Basi huyu atalazimika aendelee kufunga na mwezi wa mji wake kwa kukamilisha siku thalathini au wauone mwezi
  - Na pia shahada ya kurayb ni shahada ya mtu mmoja, na wao wameamrishwa wafanyie kazi shahada ya watu wawili katika kufungua.

Ama watu wa kauli ya tatu wamesimamishiwa hoja kwa wao kutumia dalili ya hadithi ya Kurayb kama ni hoja yenye kuwaunga mkono. Bali hadithi ya Kurayb ipo dhidi yao. Kwa sababu Mua'wiya (Allah amridhie) ndiye aliyekuwa kiongozi mkuu wa waislamu kipindi hicho na yeye alifunga mwezi wa Ramadhani na Ibn Abbaas (Allah amridhie yeye na baba yake) hakumfuata katika hilo.

(H) KUONEKANA KWA MWEZI WAKATI WA MCHANA

Ama mwezi ukionekana mchana iwe kabla ya kupinduka jua au baada ya kupinduka jua, basi unazingatiwa ni mwezi wa siku inayofuata, itawajibu kufunga ikiwa ni mwanzo wa kuingia

Ramadhani au kufungua ikiwa ni mwisho wa mwezi wa Ramadhani siku inayofuata. Na kauli hii, Imam Ibn Qudaama (Allah amrehemu) imeitia nguvu katika (Al-mughniy) na akinukuu kuwa ni kauli ya wengi katika maswahaba kama Umar, Ibn Abbas, Ibn Mas-ud na pia ni kauli ya Imam Al-auzai'i, Maalik, Shaafiy.

وعَنْ شَقِيقٍ قَالَ: كَتَبَ إِلَيْنَا عُمَرُ وَنَحْنٌ بَخَانِقِينَ: " أَنَّ الْأَهِلَّةَ بَعْضَهَا أَكْبَرُ مِنْ بَعْضٍ، فَإِذَا رَأَيْتُمُ الْهِلَالَ نَهَارًا فَلَا تُفْطِرُوا حَتَّى يَشْهَدَ رَجُلَانِ أَنَّهُمَا رَأَيَاهُ بِالْأَمْسِ

Na kutoka kwa Shaqiiq amesema; alituandikia sisi Umaru na sisi tupo Khaaniquun "Ya kwamba miezi miandamo baadhi yake ni mikubwa kuliko mingine, basi pindi mtakapouona mwezi mwandamo mchana msifuturu, mpaka washuhudie watu wawili kwamba wao waliuona jana"[13]

(I) ATAKAYE UONA MWEZI PEKE YAKE, JE! INAMLAZIMU KUFUTURU?

Atakayeona mwezi peke yake, atawajibika kufunga au kufututu. Amesema Ibn Qudaama Allah amrehem

الْمَشْهُورُ فِي الْمَذْهَبِ أَنَّهُ مَتَى رَأَى الْهِلَالَ وَاحِدٌ لَزِمَهُ الصِّيَامُ ، عَدْلًا كَانَ أَوْ غَيْرَ عَدْلٍ ، شَهِدَ عِنْدَ الْحَاكِمِ أَوْ لَمْ يَشْهَدْ ، قُبِلَتْ شَهَادَتُهُ أَوْ رُدَّتْ .وَهَذَا قَوْلُ مَالِكٍ ، وَاللَّيْثِ ، وَالشَّافِعِيِّ ، وَأَصْحَابِ الرَّأْيِ ، وَابْنِ الْمُنْذِرِ .

Na lilo mash-huri katika madh-hab (ya Imam Ahmad) ni kwamba, pindi mtu atakapouona mwezi, itamlazimu kufunga, sawa awe muadilifu au la, sawa awe ametoa ushuhuda mbele ya hakimu au la, iwe imekubalika ushahidi wake au la. Na hii ni kauli ya Maalik, na Al-layth, na Ash-shaafiy, na watu wa rai, na Ibn Al-mundhir[14]

(J) MTU AKIPEWA HABARI NA MTU ANAYE MUAMINI KUWA KAUONA MWEZI. JE! ATAFUNGA AU KUFUTURU KWA HABARI HIYO?

Mtu akipewa taarifa ya mwezi na mtu anayemuamini kuwa ameuona mwezi, basi inamlazimu kuifanyia kazi kauli hiyo, kwa kufunga ikiwa inaingia Ramadhani au kufungua ikiwa inaingia Shawwaal

إذَا أَخْبَرَهُ مَنْ يَثِقُ بِهِ كَزَوْجَتِهِ وَجَارِيَتِهِ وَصَدِيقِهِ وَغَيْرِهِمْ مِمَّنْ يَثِقُ بِهِ وَيَعْتَقِدُ صِدْقَهُ أَنَّهُ رَأَى هِلَالَ رَمَضَانَ ولم يذكر ذلك عند القضي فَقَدْ قَطَعَتْ طَائِفَةٌ بِأَنَّهُ يَلْزَمُهُ الصَّوْمُ بِقَوْلِهِ مِمَّنْ صَرَّحَ بِوُجُوبِ ذَلِكَ عَلَى الْمَقُولِ لَهُ أَبُو الْفَضْلِ بْنُ عَبْدَانَ وَالْغَزَالِيُّ فِي الْإِحْيَاءِ وَالْبَغَوِيُّ وَغَيْرُهُمْ وَقَالَ إمَامُ الْحَرَمَيْنِ وَصَاحِبُ الشَّامِلِ إنْ قُلْنَا إنَّهُ رِوَايَةٌ لَزِمَ الصَّوْمُ بِقَوْلِهِ

[13] Muswannaf Abdur razaaq Asw-swan aniy, Hadithi no. 9431
[14] Al-mughniy 4/416 (Shaamila)

Pindi (mtu) akipewa habari na mtu anaye muamini kama mkewe, na kijakazi wake, na rafiki wake na wengineo katika watu anao waamini na anaitakidi ukweli wao, ya kwamba (huyo anayemuamini) ameona mwezi mwandamo wa Ramadhani, na wala hajamwambia kadhi. Basi kundi (katika wanachuoni) limekata ya kwamba itamlazimu yeye kufunga kwa kauli yake. Katika walio weka wazi uwajibu wa hilo kwa mwenye kuambiwa ni Abul Fadhli ibn Abdaan na Al-ghazaaly katika Al-ihyaai, na Al-baghawiy na wengineo. Na akasema Imam Al-haramayn na mwenye Ash-shaamill endapo tukisema (habari yake) ni riwaya itamlazimu kufunga kwa kauli yake[15]

(K) AKIAMKA MTU AMEFUNGUA AKIITAKIDI KWAMBA NI KATIKA SHAABAN, KISHA IKASIMAMA HOJA KUWA SIKU HIYO NI KATIKA RAMADHANI NA KWAMBA MWEZI ULIANDAMA JANA

Wamekwenda wanachuoni katika mtazamo ya kuwa atafunga muda uliobakia na wala hata lipa siku hiyo, kama vile ambavyo ilivyo faradhishwa swaum ya Ashuraaa na watu wakatakiwa wafunge muda uliobakia.

عَنِ الرُّبَيِّعِ بِنْتِ مُعَوِّذٍ، قَالَتْ: أَرْسَلَ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ غَدَاةَ عَاشُورَاءَ إِلَى قُرَى الأَنْصَارِ: «مَنْ أَصْبَحَ مُفْطِرًا، فَلْيُتِمَّ بَقِيَّةَ يَوْمِهِ وَمَنْ أَصْبَحَ صَائِمًا، فَلْيَصُمْ»

Kutoka kwa Ar rubayi' bint Mu'adh, amesema: alituma ujumbe Mjumbe wa Allah juu yake sala na salamu mchana wa A'shuraa katika vitongoji vya answaar ((yeyote atakaye amka amefungua basi atimize muda ulio baki katika siku yake (yani kwa kufunga), na atakaye amka amefunga basi anaendelee na funga))[16]

(L) MTU ASIPOTAMBUA MWEZI KUANDAMA MPAKA JUA KUZAMA

Wamekwenda Jumhuri ya wanachuoni kuwa siku hiyo atailipa, kwa sababu hajaifunga na ni siku katika mwezi wa Ramadhani

(M) WAKIAMKA WATU WAMEFUNGA SIKU YA THALATHINI KATIKA RAMADHANI, KISHA IKAWAJIA WAO HABARI YA KUWA MWEZI WA SHAWWAAL UMEKWISHA ANDAMA

Wanatakiwa wafungue pindi wanapoijiwa na habari ya kuonekana mwezi, na ikiwa habari hiyo imefika ndani ya muda wa swala ya I'id basi watafungua na kuswali swala ya I'id na ikiwa habari ikiwafikia nje ya muda wa kuswali I'id basi wata swali kesho yake.

عَنْ أَبِي عُمَيْرِ بْنِ أَنَسٍ، عَنْ عُمُومَةٍ لَهُ مِنْ أَصْحَابِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، «أَنَّ رَكْبًا جَاءُوا إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَشْهَدُونَ أَنَّهُمْ رَأَوُا الْهِلَالَ بِالْأَمْسِ، فَأَمَرَهُمْ أَنْ يُفْطِرُوا، وَإِذَا أَصْبَحُوا أَنْ يَغْدُوا إِلَى مُصَلَّاهُمْ»

Kutoka kwa Umayr Ibn Anas, kutoka kwa Ami zake katika maswahaba wa Mtume juu yake sala na salamu ((Ya kwamba wapanda farasi walikuja kwa Nabii juu yake sala na salamu

[15] Al-majmuu 6/277 (Shaamila)
[16] Swahihul Bukhary, Hadithi no. 1960

wakishuhudia kwamba wao wameuona mwezi jana, akawaamrisha wafuturu na wakipambaukiwa waende kwenye muswala (sehemu ya kuswalia) wao))[17]

(N) LAU MAWINGU YAKITANDA, KISHA MTU AKAMUONA MTUME (JUU YAKE SALA NA SALAMU) USINGIZINI, KISHA AKAMWAMBIA; USIKU ULE NI KATIKA RAMADHANI

لَوْ كَانَتْ لَيْلَةُ الثَّلَاثِينَ مِنْ شَعْبَانَ وَلَمْ يَرَ النَّاسُ الْهِلَالَ فَرَأَى إنْسَانٌ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْمَنَامِ فَقَالَ لَهُ اللَّيْلَةُ أَوَّلُ رَمَضَانَ لَمْ يَصِحَّ الصَّوْمُ بِهَذَا الْمَنَامِ لَا لِصَاحِبِ الْمَنَامِ وَلَا لغيره ذكره القاضي حسين فِي الْفَتَاوَى وَآخَرُونَ مِنْ أَصْحَابِنَا وَنَقَلَ الْقَاضِي عِيَاضٌ الْإِجْمَاعَ عَلَيْهِ

Lau ukiwa usiku wa mwezi wa thalathini katika shaabani na watu hawakuona mwezi mwandamo, mtu akamuona Nabii juu yake sala na salamu katika ndoto akamwambia ya kwamba usiku huu ni mwanzo wa Ramadhani, haitosihi swaumu kwa ndoto hii si kwa muotaji au mwingineyo. Amelitaja hili Al-qadhwi Husein katik Al-fatawaa na wengineo katika watu wa madhehebu yetu, na amenukuu Al-qaadhwi I'yaadhw makubaliano ya wanachuoni katika hili[18]

(O) DUA PINDI MTU ANAPOUONA MWEZI

عن بِلالُ بْنُ يَحْيَى بْنِ طَلْحَةَ بْنِ عُبَيْدِ اللهِ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ: أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا رَأَى الْهِلالَ، قَالَ: " اللهُمَّ أَهِلَّهُ عَلَيْنَا بِالْيُمْنِ وَالْإِيمَانِ، وَالسَّلامَةِ وَالْإِسْلامِ، رَبِّي وَرَبُّكَ اللهُ

Kutoka kwa Bilal ibn Yahya ibn Twalha ibn Ubayd llahi, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake; ya kwamba Nabii juu yake sala na salamu alikuwa pindi akiona mwezi anasema (Ewe mola wetu! Tuandamishie mwezi kwa Baraka, na Imani, na salama na uislam, mola wangu na mola wako mlezi ni Allah[19]

(ii) UWAJIBU WA KUJIZUIA NA VYENYE KUFUNGUZA PINDI INAPOCHOMOZA ALFAJIR YA KWELI MPAKA KUZAMA KWA JUA

Allah mtukufu anasema

﴿ أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ ٱلصِّيَامِ ٱلرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَآئِكُمْ ۚ هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنتُمْ لِبَاسٌ لَّهُنَّ ۗ عَلِمَ ٱللَّهُ أَنَّكُمْ كُنتُمْ تَخْتَانُونَ أَنفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنكُمْ ۖ فَٱلْـَٰٔنَ بَـٰشِرُوهُنَّ وَٱبْتَغُوا۟ مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَكُمْ ۚ وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ثُمَّ أَتِمُّوا۟ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ ﴾ البقرة [187]

[17] Sunanu Abii Daud, Hadithi no. 1157
[18] Al-majmuu
[19] Musnad Ahmad, hadithi no. 1397

Mmehalalishiwa usiku wa funga kuwaingilia wake zenu, wao ni vazi lenu nanyi ni vazi lao, Allah ametambua kuwa nyinyi mlikuwa mnazikhini nafsi zenu, basi amekukubalieni toba yenu na amekusameheni, hivyo sasa changanyikeni nao na mtafute kile ambacho Allah amekuandikieni, na kuleni na kunyweni mpaka utakapo bainika utando mweupe kutokana na utando mweusi utokanao na alfajiri, kisha timizeni funga mpaka usiku

Amesema Imamul Qurtuby Allah amrehemu

جَعَلَ اللَّهُ جَلَّ ذِكْرُهُ اللَّيْلَ ظَرْفًا لِلْأَكْلِ وَالشُّرْبِ وَالْجِمَاعِ، وَالنَّهَارَ ظَرْفًا لِلصِّيَامِ، فَبَيَّنَ أَحْكَامَ الزَّمَانَيْنِ وَغَايَرَ بَيْنَهُمَا. فَلَا يجوز في اليوم شي مِمَّا أَبَاحَهُ بِاللَّيْلِ إِلَّا لِمُسَافِرٍ أَوْ مَرِيضٍ، كَمَا تَقَدَّمَ بَيَانُهُ

Amejaalia Allah (uliyetukuka utajo wake) usiku ni wakati wa kula, na kunywa, na kufanya tendo la ndoa, na (akajaalia) mchana ni wakati funga, akabainisha hukmu za zama (hizi) mbili na akazitofautisha. Basi haijuzu wakati wa mchana chochote ambacho (Allah) amekihalalisha usiku isipokuwa (amehalalisha) kwa msafiri au mgonjwa, kama ulivyotangulia ubainifu wake[20]

(iii) KUENDELEA NA NIA YA KUFUNGA MPAKA KUZAMA KWA JUA

Ukirejea katika Makala yetu no.2 katika kipengele; MTU AKINUIA KUFUNGUA KATIKATI YA FUNGA YAKE uk. 8, tumeona kuwa mtu anatakiwa nia yake aendelee nayo mpaka mwisho wa muda waswaum, na ikitokea akanuia kufungua basi swaum yake inakuwa batili, kwa hiyo ni wajibu kuwa na nia ya swaum kuanzia muda wa kufuga mpaka anapofungua mtu.

(iv) UWAJIBU WA KUTOA CHAKULA KILICHO MDOMONI KWA YULE AMBAYE UDHURU UMEONDOKA

Ama kwa yule ambaye udhuru umeondoka kwake yeye na hali ya kuwa ni mwenye kufunga, basi ina lazimika kwake yeye kutoa chakula kilicho mdomoni na kujizuia katika siku hiyo. Mfano; msafiri akifika katika mji wake, au mtoto akifikia umri wa kubalehe au kuvunja ungo, au akitwaharika mwenye hedhi au nifasi, au asipojua kuingia kwa mwezi wa Ramadhani mpaka muda wa mchana, au mgonjwa akipona. Hawa wote watahitajika kujizuia siku hii na kulipa katika masiku yajayo baada ya Ramadhani isipokuwa yule ambaye hakujua kuingia kwa mwezi wa Ramadhani, kama yalivyotangulia mas-ala yake hapo juu.

Ama mwenye kusahau kisha akala au kunywa naye pia atahitajika kutoa kilichopo mdomoni na funga yake itakuwa sahihi wala hatahitajia kulipa siku hiyo, na mas-ala yake yatakuja in shaa llah.

(v) UWAJIBU WA KUJIWEKA MBALI NA MKE AKIHOFIA KUINGIA KATIKA HARAMU

Amesema Imam An-nawawiy (Allah amrehemu)

[20] Al-jaamiu' liahkaamil Qur an 2/321 (shaamila)

قَالَ الشَّافِعِيُّ وَالْأَصْحَابُ الْقُبْلَةُ فِي الصَّوْمِ لَيْسَتْ مُحَرَّمَةً عَلَى مَنْ لَمْ تُحَرِّكْ شَهْوَتَهُ لَكِنَ الْأَوْلَى لَهُ تَرْكُهَا وَلَا يُقَالُ إِنَّهَا مَكْرُوهَةٌ لَهُ وَإِنَّمَا قَالُوا إِنَّهَا خِلَافُ الْأَوْلَى فِي حَقِّهِ مَعَ ثُبُوتِ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَفْعَلُهَا لِأَنَّهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يُؤْمَنُ فِي حَقِّهِ مُجَاوَزَةُ حَدِّ الْقُبْلَةِ وَيُخَافُ عَلَى غَيْرِهِ مُجَاوَزَتُهَا كَمَا قَالَتْ عَائِشَةُ كَانَ أَمْلَكَكُمْ لِإِرْبِهِ وَأَمَّا مَنْ حَرَّكَتْ شَهْوَتَهُ فَهِيَ حَرَامٌ فِي حَقِّهِ عَلَى الْأَصَحِّ عِنْدَ أَصْحَابِنَا وَقِيلَ مَكْرُوهَةٌ كَرَاهَةُ تَنْزِيهٍ

Amesema Ash-shaafii'yu na watu wa madhebu yake; kubusu katika swaum sio haramu kwa yule ambaye hakuamshi matamanio yake, lakini bora kwa mfungaji ni kuacha. Na wala haisemwi kuwa ni makruhu kwake, na si vinginevyo wamesema ni kinyume na bora na haki yake, pamoja na kuthibiti kuwa Nabii wa Allah juu yake sala na salamu alikuwa anafanya, kwa sababu yeye juu yake sala na salamu ilikuwa inaaminika katika haki yake kutokuzidi ukomo wa kubusu, na inahofiwa kinyume na yeye kuzidi ukomo wa kubusu, kama alivyosema Aisha "Alikuwa ni mwenye kumiliki zaidi haja yake". Na ama yule ambaye busu linaamsha hisia zake basi ni haramu katika haki yake katika kauli sahihi zaidi kwa watu wa madhehebu, na pia imesemwa ni makruhu karaha ya kutakasa[21]

(vi) UWAJIBU WA KUJIEPUSHA NA MADHAMBI

Anasema Mjumbe wa Allah (juu yake sala na salamu)

مَنْ لَمْ يَدَعْ قَوْلَ الزُّورِ، وَالْعَمَلَ بِهِ وَالْجَهْلَ، فَلَيْسَ لِلَّهِ حَاجَةٌ أَنْ يَدَعَ طَعَامَهُ وَشَرَابَهُ

Yeyote asiye acha maneno ya uongo na kuyafanyia kazi, na (kuacha) ujinga, basi Allah hana haja kwa yeye kuacha chakula chake na kinywaji chake[22]

Amesema Imam Badrud diin Al-a'iniy

فَيحْتَمل أَن يُرَاد بِالْجَهْلِ جَمِيع الْمعاصِي

Na inabebeka ya kuwa makusudio ya Aljahli (Ujinga) ni maasi yote[23]

Hivyo ni jambo la wajibu kujiepusha na maasi yote, ili swaumu ya mfugaji iwe salama mbele ya Allah (mtukufu)

(vii) JE! MAASI YANABATILISHA SWAUM?

Tumeona katika hadithi kuwa Mjumbe wa Allah (juu yake sala na salamu) amesema Allah hana haja na swaumu yake, je maana yake swaum yake ni batili?

[21] Sharhu ya sahihul muslim 7/215 (shaamila)
[22] Sahihul Bukhaary 1903
[23] Umdatul Qaarii 10/276 (Shaamila)

Amesema Imam Badrud diin Al-a'iniy

وَاخْتلف الْعلمَاء فِي أَن الْغَيْبَة والنميمة وَالْكذب: هَل يفْطر الصَّائِم؟ فَذهب الْجُمْهُور من الْأَئِمَّة إِلَى أَنه لَا يفْسد الصَّوْم بذلك، وَإِنَّمَا التَّنَزُّه عَن ذَلِك من تَمام الصَّوْم

Na wametofautiana wanachuoni katika kuteta na kusengenya na uongo, je vinamfunguza mfungaji? Wakaenda wengi katika maimam katika (kauili) ya kwamba swaum haiharibiki kwa hivyo (vitu), na si vinginevyo, kujiweka mbali na hivyo vitu ni katika utimilifu wa swaumu[24]

(viii) UWAJIBU WA KUIPENDA SWAUM YA RAMADHANI

Kufunga mwezi wa Ramadhani ni miongoni mwa mambo ambayo Allah ameyateremsha katika kitabu chake. Hivyo inahitajia mtu aipende, anasema Allah mtukufu katika kitabu chake

﴿ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمۡ كَرِهُواْ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأَحۡبَطَ أَعۡمَٰلَهُمۡ ٩ ﴾ محمد [9]

Hilo ni kwa sababu walichukia kila ambacho Allah amekiteremsha, (Allah) akayabatilisha matendo yao

Kubatilika kwa matendo yao ni kwa sababu wao wamechukia kile ambacho Allah amekiteremsha katika hukmu zake. Na kuchukia ni kinyume cha kupenda. Hivyo ni wajibu kwa kila Muislam kupenda hukmu za Allah ikiwemo swaum.

والله أعلم

Nimeikusanya usiku wa Ijumaa, Ramadhani 28 1443 – 28/04/2022

[24] Umdatul Qaarii 10/276